

TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wajumbe,

Kwanza nichukue fursa hii kuwakaribisha sana katika mkutano wetu wa Kumi na Tatu wa Baraza letu la Tisa ambao unaanza leo tarehe 6 Februari, 2019.

Waheshimiwa Wajumbe,

Napenda kutoa kwenu na kwa wananchi kwa ujumla, taarifa kuhusu Miswada ya Sheria iliyopitishwa katika Mkutano uliopita wa Baraza uliofanyika kuanzia tarehe 28 Novemba, 2018 mpaka tarehe 6 Disemba, 2018.

Katika Mkutano huo wa Kumi na Mbili wa Baraza la Wawakilishi, Baraza lilipitisha Miswada Mitatu (3) ya sheria ambayo ni:-

- 1) Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Yanayosimamia Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria, Kurahisisha Upatikanaji wa Haki na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.
- 2) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 11 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.
- 3) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Vyama vya Ushirika Nam. 4 ya Mwaka 1986 na Kutunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar ya Mwaka 2018 ambayo inaweka utaratibu wa Uundaji na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 91(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016; naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo yote niliyoitaja, sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Taarifa nyengine inahusiana na

**PONGEZI ZA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR KUHUSU MKATABA WA MGAWANYO WA
UZALISHAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA (PSA)**

Waheshimiwa Wajumbe,

Mtakumbuka kwamba miongoni mwa Hoja zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Baraza la Tisa la Wawakilishi, Zanzibar ni Hoja iliyolitaka Baraza la Wawakilishi kuunga mkono hatua ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuingia katika Mkataba wa Mgawanyo wa Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Hoja ambayo iliwasilishwa na Mhe. Nassor Salim Ali (Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni)

Waheshimiwa Wajumbe,

Baraza la Wawakilishi liliunga mkono Hoja hiyo, ambayo ilizungumzia Mkataba uliosainiwa baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya Rak Gas ya Ras Al Khaimah kwa ajili ya kufanya kazi za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika kitalu cha Pemba.

Pamoja na kuunga mkono huko, Baraza pia lilitoa maazimio makuu matatu kwa madhumuni hayo kama yafuatayo:

- i) Baraza la Wawakilishi, kwa kauli moja liunge mkono hatua ya kihistoria ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuingia katika mkataba wa mgawanyo wa Mafuta na Gesi Asilia.
- ii) Baraza la Wawakilishi kadri itakavyohitajika kwa mujibu wa Sheria, hasa kwa kupitia Kamati zake, itoe ushirikiano katika kuhakikisha kuwa Mkataba huu unatekelezwa kwa ufanisi mkubwa kwa maslahi ya Zanzibar na wananchi wake.
- iii) Baraza la Wawakilishi liendeele kuunga mkono kwa vitendo jitihada za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi za kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Waheshimiwa Wajumbe,

Baada ya kuunga mkono Hoja hiyo na maazimio yake kwa niaba yenu niliziwasilisha pongezi hizo kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumuandikia rasmi barua ya tarehe 6 Disemba, 2018 nikimueleza namna ambavyo Baraza hili Tukufu lilivyounga mkono maamuzi hayo ya Serikali. Aidha, niliambatanisha na maazimio yetu kwa mnasaba wa Hoja hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe,

Naomba nikuarifuni kwamba kwa mujibu wa barua ya tarehe 10 Disemba, 2018 yenye kumbukumbu namba IKL/TS/BLW-41/VOL.5/8 Mhe. Rais amezipokea Pongezi zetu hizo kwa dhati kabisa nae ameahidi kuyazingatia na kuyafanyia kazi maombi yetu yote yanayoendana na ushauri kuhusiana na ufanisi katika utekelezaji wa Mkataba huo wa mgawanyo wa uzalishaji wa mafuta na Gesi Asilia (PSA) kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar.

Waheshimiwa Wajumbe.

Nimeona ni vyema kuiwasilisha Taarifa hiyo ili tuendeleo kujiweka tayari katika kusaidia Serikali yetu katika kufanikisha jambo hili muhimu kwa uchumi wetu huku tukielewa kwamba Serikali yetu ipo pamoja nasi.

Waheshimiwa wajumbe nawashukuru sana.

**Zubeir Ali Maulid,
Spika,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.**

6 Februari, 2019